# MASWALI 60 JUU YA UUNGU

PAMOJA NA MAJIBU YA BIBLIA

1. Je, neno 'Utatu' liko katika Biblia? Hapana
2. Je, Biblia inasema kuwa kuna nafsi tatu katika Uungu? Hapana.
3. Je, Biblia inazungumzia juu ya Baba, Mwana na Roho Mtakatifu? Ndiyo.
4. Je, vyeo hivi kama ilivyo katika Mathayo 28:19 vinamaanisha kuna watu watatu tofauti katika Uungu? Hapana, yanarejea vyeo vitatu, ngazi au uhusiano kwa binadamu.
5. Je, Biblia inatumia neno tatu kumwelezea Mungu? Ni aya moja tu katika Biblia yote 1 Yohana 5:7. Inazungumzia juu ya Baba, neno (badala ya mwana), na Roho Mtakatifu, na inamalizia kwa kusema "Hawa watatu ni umoja).
6. Je, Biblia inatumia neno moja kumwelezea Mungu? Ndiyo, mara nyingi kwa mfano, ona Zakaria 14:9, Malaki 2:10, Mathayo 23:9, Marko 12:29,32; Yohana 8:41; 10:30; Warumi 3:30; I Wakorintho 8:4; Wagalatia 3:20; I Timotheo 2:5; Yakobo 2:19.
7. Je, Fumbo la Uungu linaweza kujulikana? Ndiyo Warumi 1:20; Wakolosai 2:9; I Timotheo 3:16.
8. Je, Mkristo ana Baba mmoja tu wa mbinguni? Ndiyo. Mathayo 23:9.
9. Basi, mbona Yesu alimwambia Filipo, "Yeye aliyeniona amemwona baba" (Yohana 14:9)? Kwa sababu Yesu ni chapa ya sura ya Mungu Waebrania 1:3. Neno la Kigiriki la kusema mtu katika aya hii ni Chapa ya nafsi yake.
10. Je, Biblia inasema kuwa kuna nafsi mbili katika Uungu? Hapana.
11. Je, Biblia inasema kwamba Uungu unafunuliwa kwa mtu mmoja? Ndiyo, katika Yesu Kristo 2 Wakorintho 4:4; Wakolosai 1:19; 2:9; Waebrania 1:3.
12. Je, siri la Uungu imefichwa kwa watu wengine? Ndiyo, Luka 10:21-22.
13. Baba ni nani? Baba ndiye Mungu mmoja, haswa ikifunuliwa katika uhusiano wa mzazi kwa binadamu. Kumbukumbu la Torati 32:6; Malaki 2:10.
14. Mungu Baba alikuwa wapi wakati Yesu alipokuwa duniani?
Baba alikuwa ndani ya Kristo. Yohana 14:10, 2 Wakorintho 5:19. Alikuwa pia mbinguni, kwa kuwa Mungu anaenea pote.
15. Je, Nabii Isaya alisema kuwa Yesu atakuwa Baba? Ndiyo Isaya 9:6; 63.16.
16. Wakati Mungu aliposema, "Na tuumbe mtu kwa mfano wetu" (Mwanzo 1:26) alikuwa anaongea na mtu mwingine kwenye Uungu? Hapana. Isaya 44:24; Malaki 2:10.
17. Ni sifa ngapi za Mungu zilikuwa kwa Kristo? Zote Wakolosai 2:9.
18. Tunawezaje kumwona Mungu aliyemtuma Yesu duniani? Kwa kumwona Yesu. Yohana 12:44-45; 14:9.
19. Je, Biblia inasema kuwa Yesu ni Mwenyezi? Ndiyo Ufunuo 1:8.
20. Ni nani ambaye watu wengine humtambua kama nafsi ya kwanza katika Utatu? Mungu Baba.
21. Ni nani ambaye watu wengine humtambua kama nafsi ya mwisho katika utatu? Roho Mtakatifu. Lakini Yesu alisema yeye ndiye wa kwanza na mwisho. Ufunuo 1:17-18.
22. Ni watu wangapi Yohana aliwaona wamekaa juu ya kiti cha enzi kule mbinguni? Mmoja. Ufunuo 4:2.
23. Kama Yesu ndiye mwanzo na mwisho kwa nini Mungu alisema katika Isaya 44:6 kwamba alikuwa ndiye wa kwanza na mwisho?
Kwa sababu Yesu ni Mungu wa Agano la Kale aliyevaa mwili.
24. Je, Yesu alimwambia shetani kuwa Mungu pekee ndiye ataabudiwa? Ndiyo Mathayo 4:10.
25. Je, Shetani anaamini zaidi ya Mungu mmoja? Hapana. Yakobo 2:19.
26. Je, Biblia inasema kwamba Mungu ambaye ni Neno, alifanyika mwili? Ndiyo, Yohana 1:1,14.
27. Ni kwa makusudi gani Mungu alidhihirishwa katika mwili? Kuwaokoa wadhambi. Waebrania 2:9,14.
28. Je, Yesu alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili? Ndiyo, I Timotheo 3:16.
29.Je Yesu aliweza kuwa duniani na mbinguni kwa wakati mmoja? Ndiyo. Yohana 3:13.
30. Je, Biblia inasema kuwa kuna Mungu mmoja? Ndiyo Isaya 45:18; Waefeso 4:5.
31. Je, Biblia inasema kuwa Kristo ni Mungu? Ndiyo. Luke 2:11.
32. Je, Biblia inasema kuwa Bwana ni Mungu? Ndiyo. I Wafalme 18:39; Zakaria 14:5; Matendo 2:39; Ufunuo 19:1.
33. Kanisa linawezaje kuwa la Yesu (Mathayo 16:18) na wakati huo kuwa kanisa la Mungu (I Wakorintho 10:32).
Kwa sababu Yesu ni Mungu katika mwili.
34. Je, Mungu atampa mwingine utukufu wake? Hapana Isaya 42:8.
35. Kulikuwa na Mungu aliyefanyika kabla ya Yehova? au kutakuwa na mwingine atakayefanyika baadaye? Hapana. Isaya 43:10
36. Ni kitu gani kimoja ambacho Mungu hafahamu? Mungu mwingine? Isaya 44:8.
37. Ni kitu gani kimoja ambacho Mungu hawezi kufanya? Kuongopa. Tito 1:2.
38. Ni Mungu wangapi inabidi tufahamu? Ni mmoja tu, Hosea 13:4.

39. Ni majina mangapi aliyo nayo Bwana? Moja, Zakaria 14:9.
40. Je, Ni vizuri kulifikiria jina la Bwana? Ndiyo. Malaki 3:16.
41. Je, Biblia inasema kuwa Mungu pekee alitembea juu ya mawimbi ya bahari? Ndiyo Ayubu 9:8.
42. Kwa nini Yesu aliweza kutembea juu ya bahari ya Galilaya (Mathayo 14:25)? Kwa sababu ni Mungu muumba Wakolosai 1:16.
43. Je, Mungu ndiye pekee awezaye kusamehe dhambi? Ndiyo. Isaya 43:25; Marko 2:7.
44. Kwa nini, Yesu alisamehe dhambi katika Marko 2:5-11? Kwa sababu ni Mungu mwokozi.
45. Je, Yesu ni Mungu wa kweli? Ndiyo. I Yohana 5:20.
46. Kama Mungu na Roho Mtakatifu ni watu wawili tofauti, ni yupi alikuwa Baba wa Kristo? Matayo 1:20 inasema kuwa Roho Mtakatifu alikuwa Baba, wakati Warumi 15:6, II Wakorintho 11:31 na Waefeso 1:3 zinasema kuwa Mungu alikuwa Baba. Hakuna upinzani wakati tukitambua kuwa Mungu Baba na Roho Mtakatifu ni wamoja na Roho mmoja. Mathayo 10:20; Waefeso 4:4; I Wakorintho 3:16.
47. Wakati Paulo alipomuuliza Bwana yeye alikuwa nani, jibu lilikuwa nini? "Mimi ndimi Yesu" Matendo 9:5.
48. Wakati Stephano alipokuwa anakufa, alimwita Mungu ni Yesu? Ndiyo Matendo 7:59.
49. Je, Tomaso aliwahi kumwita Yesu ni Mungu? Ndiyo. Yohana 20:28.
50. Yesu awezaje kuwa mwokozi, wakati Mungu baba alisema katika Isaya 43:11, "Zaidi yangu mimi hakuna mkombozi mwingine?
Kwa sababu "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake", 2 Wakorintho 5:19.
51. Je, Biblia yasema kuwa Yesu alikuwa Mungu pamoja nasi? Ndiyo Mathayo 1:23.
52. Je, Yesu aliwahi kusema, "Mimi na Baba yangu tu umoja? Ndiyo. Yohana 10:30.
53. Inaweza kuhakikishwa kimaandiko kuwa Yesu na Baba ni wamoja sawa sawa kama mume na mke walivyo wamoja. Hapana. Uungu haukulinganishwa katika uhusiano wa mume na mke. Yesu alijitambulisha mwenyewe na Baba katika njia ambayo mume na mke hawawezi kutambulikana pamoja na mwingine. Yohana 14:9-11.
54. Je, Biblia inasema kuwa kuna Mungu mmoja mwenye busara? Ndiyo. Yuda 25.
55. Je, Biblia huita Roho Mtakatifu kuwa nafsi ya pili au ya tatu katika Uungu? Hapana. Roho Mtakatifu ni Roho moja ya Mungu, ni Mungu mmoja mwenyewe akifanya kazi katika maisha yetu. Yohana 4:24; 1 Wakorintho 3:16-17; 6:19; 12:13.
56. Je, wana utatu waweza kuonyesha kuwa watu watatu wa Kimungu walikuwepo wakati Yesu alipobatizwa na Yohana? Hapana kabisa. Mungu mmoja anayeenea pote. Alikuwa mmoja mwenye kujidhihirisha. Ni nafsi moja tu ilikuwepo Bwana Yesu Kristo.
57. Basi, wale wengine wawili wanaowasema wanautatu walikuwa wakina nani? Moja ilikuwa ni sauti toka mbinguni, ingine ilikuwa Roho wa Mungu kama mfano wa njiwa. Mathayo 3:16-17.
58. Sauti ilisema nini katika ubatizo wa Yesu? "Huyu ni mwanangu mpendwa nipendezwaye naye," Marko 1:11. Kama mwana wa Mungu, Yesu alikuwa ndiye Mungu aliyevaa mwili.
59. Je, Biblia inasema kuwa Mungu alimwaga damu na kuwa alitoa uhai wake kwa ajili yetu? Ndiyo Matendo 20:28; I Yohana 3:16. Mungu aliweza kufanya hivyo kwa sababu aliweza kuchukua mwili wa kibinadamu.
60. Biblia yasema kuwa Mungu atarudi na watakatifu wake wote (Zakaria 14:5) na pia Yesu atarudi na watakatifu wake wote (I Wathesalonike 3:13). Je, ni wawili wanarudi? Hapana ni mmoja tu atakayerudi - Mungu wetu mkuu na mwokozi Yesu Kristo. Tito 2:13.

**Chapishwa na:**
**UNITED PENTECOSTAL CHURCH OF TANZANIA**
**SLP 1271**
**MOSHI, TANZANIA**